



Wende jichanjisha !

Namna gani chanjo zinatumika ?

- Kupitia chanjo, mwili wako unatengeneza kingamwili.
- Vitu hizi zinasaidia kwa kupinganisha chembe cha virusi .
- Unawasiliana na janga la virusi ya corona baada ya hapo ? Kingamwili hizi zitakulinda.

Kwa nini chanjo inashauriwa ?

- Janga la virusi ya corona ni hatari kwa kiasi ya watu wanao wasiliana nawe kwa karibu :
 - Watu wa umri ya miaka sitini na tano na zaidi.
 - Watu wanaouguwa magonjwa ya mapafu, ya moyo au ya mishipa.
 - Watu wanaouguwa magonjwa ya kisukari au shinikizo la damu.

Lakini virusi inaweza pia kua hatari kwa watu ambao ni vijana na wenye afya bora.

- Ikiwa asili mia sabini ya watu (70%) Ubeljiji wanapata chanjo, kusambaa kwa virusi kutapunguka . Ni hiyo inaitwa « kinga ya kundi »
- Maisha yako itarejesha haraka zaidi hali yake ya kawaida.
- Mwili wako utajilinda vizuri zaidi dhidi ya virusi.
- Lakini uendeleo kuheshimu maelekezo hadi watu wakutosha watapata chanjo. Heshimu umbali wa mita moja na nusu kati yako na wengine, vaa barakoa au mask yako na osha mara kwa mara mikono yako.

Chanjo itatumikishwa namna gani ?

- Utaingizwa shindano mbili ngambo ya juu ya mkono.
- Utaingizwa shindano ya pili baada ya wiki (au juma) tatu hadi inne baada ya kupokea chanjo ya kwanza.
- Baada ya shindano ya pili, inafaa kuchunga siku kumi na tano. Kiisha, chanjo itakulinda vizuri iwezekanavyo dhidi ya corona.

Chanjo ni yenye uhakika ?



- Kunakuwepo (au kunapatikana) utaaluma kumbwa kuusu jambo ya kutengeneza chanjo. Wanasayansi na wataalamu ya madawa wa dunia nzima waliwai kuendeleza chanjo katika muda mfumpi. Kulikua pia pesa ya kutosha na muda kwa kufanya kazi hiyo kwa sababu ilikua ya haraka.
- Chanjo ilikua kwanza imechunguzwa kabisa na serikali. Ni yenye uhakika kabisa.

Je naweza sikia athari (au vinyume) baada ya chanjo ?

Inawezekana usikie athari (vinyume) zifuatazo :

- Kubadilika kidogo kwa mwili kua nyekundu, maumivu au mwili kuvimba kidogo juu ya mkono (pale ulipata chanjo)
- Mchoko
- Maumivu kichwani
- Ongezeko isiyo kumbwa (au ongezeko ndogo) ya temprecha

Ni kawaida na siyo ya kutisha. Unaweza tumia paracetamol.

Wakati gani nitapata chanjo ?

- Januari :
 - Wakazi na watumishi wa vituo vya afya ya makao
 - Watumishi wa sekta ya afya (daktari, wauguzi,...) wa hospitali.
- Februari :
 - Watumishi wa sekta ya afya wanao husika na matibabu ya msingi (daktari wa jamaa, wafamasia,...)
 - Vituo vya afya ya umma (sekta ya usaidiaji kwa watu wenye ulemavu,...) na watu wanao tumika hospitalini.
- Mach :
 - Watu wa umri ya miaka sitini na tano au zaidi.
 - Watu ambao wanakua katika hatari kumbwa kulingana na afya yao.
- Aprili :
 - Watu wanao tumika kazi ya muhimu sana.
- Tangu juni :
 - Mtu yeyote yule ambaye ana zaidi ya umri wa miaka kumi na nane.

Kalenda hii inaweza tena badilika.



Watu wamoja hawawezi pata chanjo. Kwa mfamo: wagonjwa wanaokumbwa na kansa, wanawake wajawazito au watu wanao sumbuka mno na mizio. Kwa taarifa zaidi, wasiliana na daktari wako.

Namna gani nitajua muda ambayo nitapata chanjo (au muda ambayo nitachanjwa) ?

- Utapokea mwaliko kupitia barua, ujumbe mfupi na au barua pepe.
- Utajiorodhesha kupitia teknolojia ya kompyuta au kupitia simu.
- Muda aikufuraishi ? Ikiwa ni ivyo, unaweza chagua muda ingine.
- Ikiwa autoe maoni yako, mji au mtaa wako utawasiliana nawe.

Ni wapi ambapo naweza kujichanjisha ?

Katika kituo cha chanjo.

Na chanjo hii ni ya gharama ngapi ? (au chanjo hii inauzishwa ngapi ?)

Chanjo inatolewa bure (bila gharama yoyote)

Kwa taarifa zaidi, fungua ?

<https://www.laatjevaccinieren.be/>

<https://www.info-coronavirus.be/fr/vaccination/>